# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI

ISSN 2507-797X Toleo No 2 2023/2024

## "KARIBU KINONDONI"

## KINONDONI INAPENDEZA




# Tumeahidi na Tunatekeleza, Uwekezaji Bora kwa Manufaa Makubwa ya Nchi Yetu






**MHARIRI MKUU**
**AQUILINUS SHIDUKI**

**MHARIRI MSAIDIZI**
**BEATA SINGANO**

**WAPIGA PICHA**
**KAUNGA MAULID**
**SAUMA MWANSHULI**

**MSANIFU JARIDA**
**KAUNGA MAULID**

**JARIDA LIMETOLEWA NA**
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**
**S.L.P KINONDONI, 31902 DSM**
**SIMU: +255222170173**
**BARUA PEPE: md@kinondonimc.go.tz**



# BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 135



*Baadhi ya Madiwani kutoka kata 20 za Halmashauri ya Mnaispaa ya Kinondoni wakitoa maoni yao na kupitisha bajeti kwa mwaka 2023/2024 ya Shilingi bilioni 135,891,778,000.00.*

**Na AQUILINUS SHIDUKI**

BARAZA la Madiwani la Manispaa ya Kinondoni, limepitisha mapendekezo ya bajeti kwa mwaka 2023/2024 ya Shilingi bilioni 135,891,778,000.00.

Katika kikao maalum kilichoketi hivi karibuni chini ya Mwenyekiti ambaye ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Mhe. Songoro Mnyonge amesema bajeti hiyo ina ongezeko la asilimia 8 ya makusanyo ya ndani ya bajeti ya mwaka 2022/2023 inayoendelea kutekelezwa. katika bajeti ya mwaka 2022/2023 bajeti ya mapato ya ndani ni Shilingi 57,210,679,000.00 huku matarajio ya bajeti ya makusanyo ya ndani yatakuwa ni Shilingi 61,605,932,000.00 ikiwa ni ongezeko la shilingi 4,395,253,000.00.

Katika makisio ya bajeti ijayo, Serikali Kuu inatarajiwa kutoa ruzuku ya Shilingi 74,285,846,000.00 ambayo ni sawa na asilimia 55 ya bajeti nzima ya Manispaa.

Katika bajeti hiyo. Mapato ya ndani ya Manispaa yatachangia asilimia 45 ya bajeti nzima.

Mstahiki Meya aliwaeleza wajumbe wa Baraza hilo Maalum kuwa, "bajeti hii imegusa kila Kata katika Manispaa yetu, imejielekeza katika utekelezaji wa miradia ya maendeleo nakama tutakusanya vizuri mapato, tutaiwekla sehemu nzuri Manispaa yetu," na kuongeza "kwa ongezeko hili la bajeti ya makusanyo ya ndani, tunazidi kuimarika na lengo ni kujitegemea."

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, alilishukuru Barala hilo kwa kuunga mkono na kuipitisha bajeti hiyo. Alilieleza Baraza hilo Maalum kuwa Manispaa ambayo ni watekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM imejipanga vizuri katika ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha wa 2023/2024.




*"Kinondoni bila Unyanyasaji Inawezekana"*



**Bi. STELLA MSOFE**

**Katibu Tawala Manispaa ya Kinondoni**

Katika kuelekea siku ya wanawake Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 8, kila mwaka ya Mwezi wa pili, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inapenda kutoa pongezi za dhati kwa watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

"Katika maadhimisho hayo tuungane kwa pamoja kutokomeza masuala yote ya unyanyasaji ndani ya Manispaa ya Kinopndoni,".

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inawatakia maadhimisho mema watumishi pamoja na wananchi wake kwa ujumla.

***"Happy Women Day"***

# WALIOFAULU KIDATO CHA KWANZA WATAKIWA KURIPOTI SHULE KABLA YA HATUA HAZIJACHUKULIWA



**Wavulana 7,377**

**Wasichana 7,448**

**Waliofaulu kidato cha Kwanza 2023 Manispaa ya Kinondoni 14,845**

Na
**SAUMA MWANSHULI**

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule ametoa wito kwa wazazi na walezi Manispaa ya Kinondoni kuwapeleka shuleni watoto wao waliofaulu kidato cha kwanza kabla ya hatua kali hazijachukuliwa.

Hayo yalizingumzwa katika kikao cha ushauri wa bajeti ya mwaka 2023/2024 ambacho kiliudhuliwa na wajumbe mbalimbali ikiwepo madiwani na watendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na kukubaliana na bajeti hiyo.

“Niwaombe kila mzazi, mlezi au jirani mwenye mtoto aliyefaulu kwenda kidato cha kwanza ahakikishe anampeleka shule mtoto huyo kabla ya tarehe 13 ya mwezi huu wa pili,” amesema Mhe. Saad.

Mbali na hayo pia Mhe Saad amehimiza wazazi hao pamoja na viongozi wa kata kuhakikisha wanatoa lishe bora kwa watoto hao ili kuwaimarisha kiakili na kiafya.

Hata hivyo Mhe. Mtambule aliwataka wafanyabiashara wakiwepo mamantilie na wamachinga kuzingatia sheria na taratibu na maelekezo yanayotolewa ili kuimalisha usalama kwa kila mtu ndani ya Manispaa ya Kinondoni.

“Nitoe wito kwa wanakinondoni hasa wanao fanya biashara ndogo ndogo na wanauza vyakula wakati serikali inaboresha miundombinu mbalimbali tuhakikishe tunazingatia sheria na taratibu na maelekezo yanatolewa ili shughuli za uboreshaji uendelee,” amesema Mhe. Saad.

Vilevile Mhe. Saad amesema Serikali imekuwa ikiingia ghrama kubwa ya kufanya kurekebisha barabara ambazo zimekuwa zikiharibiwa na magari yenye uzito zaidi ya tani 10.

Pia Mkuu wa Wilaya huyo amesema mitaro mingi ya barabara za Manispaa ya Kinondoni imezibwa na wafanyabiashara hasa wapika chipsi wanaomwaga uchafu kwenye mitaro hiyo.

“Niawombe wakazi wa Kinondoni kuendelea kutunza barabara za mtaa na kuhakikisha magari yenye uzito zaidi ya tani kumi zisipite kwenye barabara hizo, pamoja na wafanyabiashara wanauza chipsi na chakula kutogeuza mitaro ya barabara hizo kuwa kalo za maji machafu,” amesema Mhe. Saad.

# DAS KINONDONI: MSIOGOPE KUKEMEA UKATILI WA KIJINSIA

**Na KAUNGA MAULID**

Wajumbe wa Kamati ya Kudhibiti Ukatili wa Kijinsia Manispaa ya Kinondoni, wametakiwa kutoogopa kufuatilia vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Rai hiyo imetolewa na Katibu Tawala Wilayaya Kinondoni, Bi. Stella Msofe, katika kikao cha pamoja kilichojumuisha maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa Januari 21, 2023. Kikao hicho kilishirikisha Viongozi wa Dini, wazazi, Maofisa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, SIMAUJATA na Watendaji wa Kata.

Bi. Msofe alisema, "kuendelelea kujitokeza kwa taarifa nyingi za ukatili wa kijinsia na kwa watoto ni matokeo ya kuwepo kwa ufahamu kwa jamii dhidi ya vitendo hivi," alisema na kuongeza kuwa, "inawezekana zamani uelewa haukuwa mkubwa sana na ndiyo sababu za kutojitokeza kwa wingi kwa taarifa hizo."

Alisisitiza kuwa, kila mmoja kwa namna yake



*Katibu Tawala wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni akiongea katika kikao cha pamoja kilichojumuisha maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa.*

anatakiwa kujua nafasi na mchango wake katika kupinga ukatili wa kijinsia na kwa watoto. Alisisitiza kuwa, "tusifiche ukatili ndani ya familia, viongozi wa Dini kemeeni ndani ya nyumba za ibada." Aliwataka wajumbe wa kikao hicho kila mmoja kutoka akiwa na mbinu za kupambana na ukatili wa kijinsia.

Naye Mwenyekiti wa SIMAUJATA Wilayaya Kinondoni, akichangia katika kikao hicho aliwasihi washiriki kutokata tamaa katika kupinga ukatili wa kijinsia. Alisema kuwa, "tukubali kuwa ukatili wa kijinsia upo na hivyo tukubali kuukataa ukatili huo na tuendelee kutoa taarifa kwa vyombo vya Sheria ili hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika. Hata hivyo, mweyekiti huyo aliishauri Serikali kuwawezesha vijana ili waendelee kufuatilia, kutoa taarifa na kukemea ukatili wa kijinsia.

Awali, Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Kinondoni, Bw. Alex Ntiboneka, alimweleza Katibu Tawala huyo kuwa, kikao hicho kina lengo la kuwezeshana na kubadilishana uzoefu katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.



# TAHARIRI

## HONGERA MADIWANI KWA KUPITISHA BAJETI 2023/2024



Wakati Idara na Mamlaka za Serikali ya Mitaa zikiwa katika maandalizi ya bajeti ya mwaka 2023/2024, Baraza la Madiwani la Manispaa ya Kinondoni katika kikao chake Maalum limeunga mkono na kupitisha makisio ya bajeti ya Manispaa ya jumla ya Shilingi 135,891,778,000.00.

Bajeti iliyopitishwa na Baraza hilo inaongezeko la asilimia Nane (8%) ya makusanyo ya ndani ya bajeti ya mwaka 2022/2023 inayoendelea ambayo inatoka Shilingi 57,210,679,000.00 na kuwa na kiasi tarajiwa cha Shilingi 61,605,932,000.00 ikiwa ni ongezeko la shilingi 4,395,253,000.00. Serikali Kuu inatarajiwa kutoa ruzuku ya Shilingi 74,285,846,000.00 ambayo ni sawa na asilimia 55 ya bajeti nzima ya Manispaa. Katika bajeti hiyo. Mapato ya ndani ya Manispaa yatachangia asilimia 45 ya bajeti nzima.

Tunalipongeza Baraza la Madiwani kwa uamuzi wake wa kuiunga mkono na kuipitisha bajeti hii. Bajeti hii ina mwelekeo wa kukamilisha na kuanza miradi mikakati mingine mipya ya maendeleo ndani ya Manispaa. Kwa uchache, miradi mikakati inayoendelea kutekelezwa katika Manispaa yetu ni pamoja na Uwanja wa Mpira na Kituo cha Daladala vyote vikiwa Mwenge; ukamilishaji wa jengo jipya la Ofisi; Ujenzi wa Kituo cha Mabasi ya Mkoani kinachotarajiwa hapo Tegeta na miradi mingine.

Kama ilivyokuwa kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 ambapo makusanyo ya ndani yalifikia asilimia 97 ya lengo, ni imani yetu kuwa chini ya uongozi na usimamizi wa Baraza la Madiwani kwa kushirikiana na wataalam na watendaji wote, makusanyo ya ndani kwa mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 ya takribani Bilioni 61 yatafikiwa kwa asilimia 100. Vivyo hivyo kwa makusanyo ya ndani kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Kama alivyogusia Mstahiki Meya kuwa bajeti hii imegusa kila Kata ni hakika, makisio ya bajeti ijayo hususan makusanyo ya ndani ambayo asilimia 70 inakwenda kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, imejielekeza kutatua kero za wananchi.

Shime sasa kwa wananchi wa Manispaa ya Kinondoni kuendelea kuunga mkono juhudi hizi za Manispaa kwa kuendelea kulipia tozo mbalimbali ili Manispaa ikusanye mapato na kuzipeleka fedha hizo kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.







# DC MTAMBULE: ULINZI NA USALAMA NI JUKUMU LETU



## ASANTENI JESHI LA POLISI



**Na AQUILINUS SHIDUKI**

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni amelihakikishia Umma na wakazi wa Kinondoni kuwa suala la Ulinzi na Usalama wa raia ni la kipaumbele.

"Naomba niwatoe hofu wakazi wote wa Kinondoni kuwa suala la ulinzi ni Kipaumbele çhangu.

Natoa wito kwa vijana wote wanaojiita panya road, ukanda huu hakuna utakapojificha tusikukamate. Ukañda huu si salama kwenu." DC Saad alisema.

Aidha amewataka wananchi kuhakikisha wanasaidiana na Jeshi la Polisi ili maeneo yote yanakuwa salama. "Polisi endeleeni kuimarisha ulinzi, hakuna kulala Wala kupumzika ili maeneo yetu yawe salama."

"Wazazi na walezi hakikisheni mnatoa malezi mazuri kwa watoto. Aidha natoa onyo kwa wananchi wanaotoa taarifa za uongo zenye kuleta taharuki, hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Toeni taarifa sahihi na sisi tutakuja hapo haraka iwezekanavyo ili kuokoa maisha ya watu.'

Mkuu wa Wilaya ameyasema hayo leo katika Mkutano wa badhara uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Bunju 'A' kufuatia taarifa za uzushi za uwepo wa vijana wahalifu maarufu Kama Panya road.

Kwa upande wao Wakuu wa Polisi Kawe na Mapwebande wamesema kuwa Jeshi la Polisi lipo tayari kukabiliana na Jambo lolote la uhalifu litakalojitokeza. Aidha wamewataka wazazi na walezi kusaidiana na Jeshi hilo kuwafichua vijana wahalifu ili kuwadhibiti mapema.

Nao wa Mitaa ya Kata za Mbweni, Bunju na Wazo Wilaya ya Kinondoni wamemuelezea Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Saad Mtambule kuwa hakuna tukio Wala tishio la panyaroad lililojitokeza katika maeneo yao.

"Tunakuhakikishia kuwa maeneo yetu kwa siku ya Jana yalikuwa salama kabisa," alisema Bw. Zimwi ambaye Ni Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Mitaa Wilaya ya Kinondoni.

*"Wazazi na walezi hakikisheni mnatoa malezi mazuri kwa watoto, ".*



# RC MAKALA AWATAKA WAKUU WA WILAYA KUSIMAMIA MAPATO



**Na AQUILINUS SHIDUKI**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Amos Makala, amewataka Wakuu wa Wilaya wapya kusimamia mapato katika wilaya zao.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa kuwatambulisha wakuu hao wa wilaya katika kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa Anatouglo, Manispaa ya Ilala. Alisema, "simamieni mapato, mapato yawe kipaumbele chenu, mapato yanawezesha kuhudumia wananchi na kutekeleza miradi ya maendeleo."

Akifafanua zaidi majukumu ya wakuu hao wa wilaya katika wilaya zao mpya, Mheshimiwa Makala pia aliwataka wakuu hao kusikiliza na kutatua kero za wananchi, kusimamia ulinzi na usalama wa wananchi na kuhimiza usafi katika maeneo yao ya kazi. Mheshimiwa Makala aliongeza kuwa, "fuatilieni miradi ya maendeleo, muifahamu na muikague mara kwa mara."

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, alifanya mabadiliko ya Wakuu wa Wilaya na kuteua wengine wapya. Miongoni mwa waliobadilishiwa vituo vya vya kazi ni pamoja aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Mhe. Saad Mtambule ambaye amehamishiwa Wuilaya ya Kinondoni huku Mheshimiwa Godwini Gondwe akitoka Kinondoni kwenda wilaya ya Bahi. Kwa upande wao, Wakuu wa Wilaya wamemuhakikishia Mheshimiwa Makala utendaji kazi kwa bidii, uadilifu na kusikiliza kero za wananchi.

Katika makabidhiano ya Ofisi Mheshimiwa Mtambule ambaye ni Mkuu mpya wa Wilaya ya Kinondoni, amebainisha vipaumbele vyake kwa uchache kuwa ni pamoja na kusimamia elimu, Lishe, usafi, ukusanyaji na matumizi sahihi ya mapato, ulinzi na usalama wa wakazi wa Kinondoni na kuzuia ukatili kwa makundi maalum.

Alisema kuwa, "tutaimarisha ulinzi na usalama wa watu wetu, hatutaki kusikia kuna ukatili kwa wanawake na watoto wala watu kuishi kwa wasiwasi. Tutahakikisha tunadhibiti vitendo viouvu vikiwemo vya madawa ya kulevya."

Aliwataka watumishi wa Manispaa ya Kinondoni kuwahakikisha wanaendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi na kudhibiti matumizi yake.

Mheshimiwa Mtambule pia aliwataka watumishi wa Manispaa ya Kinondoni kuongeza weledi katika utendaji kazi wao. Alisema, "tuonhgeze weledi na juhudi katika kazi zetu. Kila mtumishi akiongeza weledi, tutaleta tija kwa wananchi tunaowahudumia na kuongeza thamani ya kazi"

## "PIGENI KAZI, TUMSAIDIE MAMA"



# "WATENDAJI SIMAMIENI LISHE MASHULENI"



Na
**KAUNGA MAULID**

Watendaji wa kata zote za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni wametakiwa kusimamia na kutoa elimu juu ya lishe kwa watoto wa shule za msingi na sekondari.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi Hanifa Suleiman Hamza wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za lishe kwa robo ya pili Octoba hadi Disemba 2022.

"Lishe ni jambo muhimu sana katika ngazi ya ukuaji kwa watoto wetu hivyo watendaji wa kata zote za Halmashauri yetu nawaomba mkasimamie na kutoa elimu ya kutosha kwa wazazi pamoja na watoto wenyewe mashuri juu umuhimu wa lishe bora," amesema Bi. Hanifa.

Bi. Hanifa amesema kuwa "taarifa hii inaonesha mwelekeo mzuri wa kile kilichotarajiwa hapo awali na ni mda muafaka kuangalia mambo ya msingi ili tufikie kwenye lengo mahususi".

Aidha Bi. Hanifa amewahimiza Watendaji hususani wanaofanya kazi ngazi za Kata kuendelea na jitihada za kuwatembelea, kuwahimiza na kuwapa elimu walengwa wote, " elimu juu ya umhimu wa lishe inatakiwa itolewe kwa nguvu zote ili watu waone uzito na umhimu wake" ameongeza Bi. Hanifa.

Akiwasilisha taarifa hiyo kwa niaba ya Katibu wa Kamati Bi Emilliana Sumaye amesema kuwa Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa kwa kipindi hiki pia kuna changamoto zinazotakiwa kutatuliwa ili malengo tarajiwa yatimizwe.

Lakini pia Bi. Hanifa wakati akipokea taarifa hiyo ya utekelezaji wa shughuli za lishe kwa robo ya pili Octoba-Disemba 2022 amepongeza utekelezaji uliofanyika kwa kipindi husika.






TUFUATILIE KUPITIA MITANDAO YETU YA KIJAMII

kinondonimunicipal

@kinondonimc1

kinondonimunicipalcouncil

KMC Onlinetv



# USAFI NDIO DIRA YA MAENDELEO

Na
KAUNGA MAULID

Moja ya mikakati ya kuboresha na kukuza maendeleo ya Manispaa ni kuweka mikakati ya pamoja yenye dira ya maendeo ndani ya jamii husika.

Katika mikakati hiyo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono na sera za serikali ili kuhakikisha zoezi la usafi ni madhubuti katika kuleta maendeleo.

Hivi karibu takwimu zilitoka na kuonesha kuwa Jiji la Dar es Salaam limekuwa nafasi ya tano kwa usafi barani Africa na hii imekuwa ikichagizwa na jitihada za viongozi wetu ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Licha ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amosi Makala kuweka sheria ya kufanya usafi kila Jumamos ya Mwisho wa mwezi ambayo imekuwa ikienda sambamba na kauli mbiu isemayo "Pendezesha Dar es Salaam, Safisha Dar es Salaam" huku Manispaa ya Kinondoni imekuwa na kauli mbiu isemayo ""“Pendezesha Kinondoni, Safisha Kinondoni”.

Hivi karibuni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetoa rai kwa wafanyabiashara ndani ya Manispaa



hiyo kurudi kwenye maeneo yaliyopangwa na yanayotambulika na Manispaa kibiashara ili kuzuia uchafuzi wa Mazingira.

Rai hiyo imetolewa na Katibu Tawala wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Stella Msofe wakati wa zeozi la usafi lililofanyika eneo la Mbezi Juu jijini Dar es Salaam huku likiongozwa na viongozi mbalimbali wa Serikali pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Abbas Mtemvu na viongozi wa shina kutoka mkoani.

" N i w a o m b e wafanyabiashara kutoka maeneo ya Manispaa ya Kinondoni kurudi katika maoeneo yao kama walivyokuwa. wamepangwa na kuelekezwa kwani sasa hivi kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wafanyabiashara hasa maeneo ya Tegeta kwa Ndevu wameanza kuweka biashara zao barabarani," amesema Bi. Msofe.

Lakini pia Bi. Msofe amewaomba wananchi wa Kata ya Mbezi juu na wanakinondoni kwa ujumla kuwa na utamaduni wa kufanya usafi katika maeneo yao kila siku na wasisubiri hadi siku ya mwisho wa mwezi.

## USAFI NI JUKUMU LETU SOTE







# KINONDONI YAAHIDI KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI ZOTE NCHINI ILI KUONGEZA MBINU ZA UKUSANYAJI MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI.

**Na SAUMA MWANSHULI**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yaahidi kushirikiana kwa pamoja na Halmashauri zingine katika kubuni na kuendeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kukuza mapato ya ndani ya Manispaa husika.

Hayo yamesemwa na Naibu Meya Manispaa ya Kinondoni Mhe. Joseph Rwegasira leo Februari 10, 2023 wakati akiwapokea viongozi mbalimbali kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji waliokuja kwa ajili ya kujifunza namna ya Manispaa ya Kinondoni inavyofanikiwa katika ukusanyaji wa mapato kupitia mradi wake wa mbolea ya asili uliopo kata ya Mabwepande.

"Kwa dhati kabisa kutoka moyoni mwangu kwa niaba ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni tunaahidi kushirikiana kwa dhati kabisa na Manispaa ya Kigoma Ujiji na Manispaa zingine zote nchini ambazo zitaona umuhimu wa kushirikiana katika kubadilishana ubunifu na mbinu mbalimbali zitakazonyenyua ukusanyaji wa mapato ya ndani kama ambavyo tumekuwa tukiongoza kwa ukusanyaji wa mapato ya nadani," amesema Rwegasira.

**Akiongea kuhusu bei ya mbelea hiyo Bw Hija amesema kuwa mbolea hiyo inauzwa shilingi 300 kwa kilo moja ambapo kwa tani 1 amnbayo ni kilo 1000 inauzwa shilingi 300,000/- japo bado iko kwenye majaribio**

Hata hivyo Mhe. Rwegasira amesema mradi huu wa mbolea asili umekuwa na manufaa makubwa sana ndani ya Manispaa yetu ya Kinondoni kwani lengo kubwa la mradi huu umejikita zaidi katika kutunza mazingira na kuhakikisha mazingira yetu yako safi muda wote.

Pia Naibu Meya amesema kuwa uzalishaji wa mbolea hiyo ya asili itaenda kuwanufausha wakazi wa Manispaa hii pamoja na kuongeza pato la ndani ya Manispaa kwani uhitaji wa mbolea hii umeanza kuwa wenye kasi kutokana na matokeo yake kuwa chanya kwa wakulima wengi wanaotumia mbolea hiyo.





Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Bw. Saleh Hija amesema kuwa kiwanda hicho kinauwezo wa kuzalisha tani 50 kwa siku ambpo kwa mwaka kiwanda hicho kinazalisha Zaidi ya tani 18,000.

# BIASHARA NA UWEZESHAJI

## Karibu Malolo Ujifunze Kulima na Kufuga Kisasa kwa Maendeleo Yetu



*Tunawezesha vikundi mbalimbali, Vijana, Wamama Pamoja na Vikundi vya Watu Wenye Ulemavu*











# VIKUNDI VYAASWA MATUMIZI SAHIHI YA MIKOPO

**Na AQUILINUS SHUDUKI**




Vikundi 115 vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu vimeaswa kutumia vizuri mikopo ya asilimia Kumi inayotolewa na Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya kukuza uchumi, kuongeza kipato na kutengeneza ajira.

Kauli hiyo, imetolewa Februari 18, 2023 na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Mhe. Saad Mtambule, wakati wa halfa ya utoaji mikopo yenye jumla ya Shilingi 2,555,333,322. Vikundi vilivyonufaika na mikopo hiyo ni vikundi 11 vya walemavu walioapata shilingi 297,754,580; Wanawake vikundi 73 vilivyopata Shilingi 1,239,150,000 na Vijana vikundi 31 ambao wamepata Shilingi 1,018,428,742.

Mheshimiwa Mtambule alisema, "Manispaa imetekeleza jukumu lake la kisheria la kutoa mikopo isiyo na riba kwenu, hivyo ni jukumu lenu kuwajibika kutumia mikopo hii vizuri ili mpate faida, mkuze uchumi na kutengeneza ajira. Simamieni vizuri biashara zenu ili mrejeshe mikopo yenu na msimkatishe tamaa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Chama cha Mapinduzi na Manispaa yenu," Aidha aliwataka wanufaika hao kutoielekeza mikopo hiyo kwenye shughuli zisizo kusudiwa. Pia aliwataka wanufaika kufanya bishara katika mazingira salama na safi.

Katika hatua nyingine, Mheshimiwa Mtambule ameipongeza Manispaa ya Kinondoni kuwa kutoa mikopo ya asilimia Kumi kwa utimilifu. "Kuna Halmashauri nyingi nchini hazifikii malengo ya utoaji mikopo hii kwa utimilifu, Lakini Manispaa hii imekuwa inaongoza kuwa kutoa mikopo. Nawapongeza sana."

Akitoa taarifa ya utoaji mikopo hiyo tangu mwaka 2017/2018, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Bi. Hanifa Suleiman Hamza, alimweleza Mkuu wa Wilaya kuwa mikopo hiyo ni ya kipindi cha robo ya kwanza na ya pili na kwamba, "halmashauri itaendelea kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo ili kufikia azma ya jamii kujikwamua kiuchumi na kupiga vita umaskini."

Alieleza kuwa halmashuri inaendelea na jitihada za kuhamsisha jamii kuunda vikundi na kuvisajili ili kuweza kupata mikopo isiyo na riba kupitia fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya asilimia Kumi ya mapatao ya ndani pamoja na pesa inayotokana na marejesho.

Naye Naibu Meya, Mheshimiwa Josephat Rwegasira, alivitahadharisha vikundi vinavyo toweka baada ya kupata mikopo kuacha tabia hiyo mara moja. "Kuna vikundi chechefu, vikishapata mikopo vinayeyuka. Tabia hii iachwe," alisema Mheshimiwa Rwegasira.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Kunduchi, Mheshimiwa Michael Urio, alionya baadhi ya watu wanaowatumia wanawake na vijana kuunda vikundi na kujipatia fedha huku walengwa wakiachwa bila kupata mikopo hiyo. Alivitaka vikundi hivyo kujiinua kiuchumi ili viondokane na mikopo.

Katika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023, Manispaa ya Kinondoni imetenga jumla ya shilingi 4,682,514,600 ambayo ni asilimia Kumi ya mapato ya ndani kwa mgawanyo wa 4:4:2 ambapo wanawake ni Shilingi 1,873,005,840, Vijana Shilingi 1,873,005840 na Watu wenye Ulemavu Shilingi 936,502,920.

# KAYA 2,344 ZAHITIMU MAFUNZO YA TASAF

**Na AQUILINUS SHIDUKI**

Jumla ya Kaya 2,344 ambazo zimekuwa kwenye mpango wa TASAF kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi Desemba 2022 zimehitimu na hivyo kuondolewa kwenye dirisha la malipo baada ya malipo ya mwisho ya mwezi Novemba na Desemba 2022.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Ofisi ya Mratibu wa TASAF pamoja na kuhitimu kwa kaya hizo, itaendelea kuwahudumia katika masuala mbalimbali pindi itakapo hitajika ikiwemo kuwapa elimu ya kuunda vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza na kuwanuganisha katika fursa mbalimbali.

Taarifa hiyo, iliyosainiwa na Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Bw. Alex Ntiboneka, imefafanua kuwa TASAF pia itandelea kufanya ufuatailiaji kwa kushirikiana na idara nyingine kwa kutoa utaalamu kwa kaya za Walengwa zilizohitimu ili wajiimarishe kiuchumi ikiwemo kuomba mikopo ya asilimia 10 kutoka Manispaa.

Aidha taarifa hiyo imeeleza zaidi kuwa tangu kuigawa Manispaa ya Kinondoni iliyoizaa



Manispaa ya Ubungo mwaka 2016 ambapo ilibakiwa na walengwa 4.040, walengwa wamekuwa wakipungua kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kujitoa , kuondolewa baada ya kukosa sifa, kuhama, vifo na uhakikiunaofanywa mara kwa mara. Hata hivyo baadhi ya manufaa yaliyopatikana nai poamoja na:

Kaya 2,133 kunufaika kupitia mpoango huu ikiwemo kuanzisha biahsra na kufanya shughuli za kilimo na usindikaji;

Jumla ya watoto (wanafunzi) 4,730 kufanikiwa kuhudhuria masomo na wengine 3,734 kuhudhuria Kliniki.

Jumla ya wanafunzi 25 kupatiwa barua za utambulisho kwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambapo mnufaika hupata mkipo kwa urahisi na kwa asilimia mia moja.

Tangu mwaka 2021 kumefanikiwa kuundwa kwa vikundi 182 vya kuweka na akiba na kuweka akiba yenye jumla ya shilingi 83,851,000.00 na kukopeshana shilingi 28,456,000.00

Vikundi viwili vimenufaika na mikopo ya asilimia 10 yenye thamani ya shilingi 15,000,000 na vikundi vingine vipo kwenye utaratibu wa kupata mikopo hiyo.

Kushiriki katika maonesho ya Nane Nane ambapo kikundi cha Mabwepande walioonesha uzalishaji inzi chuma (Black Fly Soldiers) na kikundi cha Tupendane cha Kigogo kilishiriki maonesho ya Sabasaba ya uzalishaji bidhaa, na kuboresha nyumba zao na kuzipangisha kwa lengo la kuongeza kipato.



# MEYA: VIONGOZI WA MASOKO SAIDIENI KUTAFSIRI SHERIA, TUSIOGOPE CHANGAMOTO

**Na KAUNGA MAULID**

Wafanyabiashara katika masoko 16 ya Manispaa ya Kinondoni, wameridhia kuanza kulipia tozo mpya kuanzia Februari Mosi, 2023.

Makubaliano hayo yamefikiwa katika kikao cha pamoja baina ya Uongozi wa Manispaa ya Kinondoni chini ya Mstahiki Meya, Mheshimiwa Songoro Mnyonge, na Viongozi wa Masoko kilichoketi Januari 16, 2023 katika ukumbi wa Manispaa.

Akitoa ufafanuzi wa kuanza kutumika kwa tozo hizo, Mstahiki Meya, Mheshimiwa Mnyonge, aliwaleza wafanyiabashara hao kuwa mabadiliko hayo yanatokana kuanza kutumika kwa Sheria ndogo ya Manispaa iliyopitishwa mwaka 2019.

Alisema kuwa licha ya kuidhinishwa kipindi hicho, Sheria hii haikuanza kutumika mara moja kutokana na kuona hali za kibiashara za wafanya biashara hao kuwa hazijakomaa.

Mheshimiwa Meya alisema, "Kutokana na mabadiliko ya kimfumo wa makusanyo ya tozo yanayotaka kutumika kwa mfumo wa TAUSI kwa mujibu wa Sheria, inatulazimu kukusanya tozo hizo nakama hatutakusanya kwa mfumo mpya,, mfumo huu utaonesha kuwa kuna kutokukusanywa kwa fedha na hivyo lazima tuwajibike."

Aliongeza kuwa, "mabadiliko haya siyo siri, hivyo ni lazima viongozi muwe nayo, muyafahamu ili tutakapoanza utekelezaji kusiwepo na migongano.

Mstahiki Meya aliwaeleza viongozi hao kuwa kama Sheria imeshawekwa, wafanyabiashara wote ni lazima kuitekeleza na kwamba Manispaa lazima iweke mazingira wezeshi ya na ya ushindani sawa kwa wafanyabiashara wote.

Aidha aliwahimiza Viongozi wa Masoko kuhakikisha wanasaidia kutafsiri Sheria Mpya kwa wafanayabiashara wanaowaongoza katika masoko yao.

Aidha kwa upande wao baadhi ya viongozi wa masoko, akiwemo Bw. Omar Said Ndaka wa soko la Kisiwani, alielezea baadhi ya changamoto zinazowakabili zikiwemo za uwepo wa wanyabiashara nje ya masoko hali inayoleta ushindani usio sawa wa kibiashara na kuiomba Manispaa kuitatua changamoto hiyo.

"Uwepo wa wafanyabiahsra nje ya masoko unainyima Manispaa mapato pia inaleta ushindani wa bei. Tunaomba mliangalie hili."

Aidha Bw. Juma Hamza, kutoka Soko la Tegeta nyuki, aliomba Manispaa kuharakisha uandaaji wa Mikataba baina yao na Manispaa ili kurahisisha uendeshaji wa biashara katika soko hilo ikiwemo na uboreshaji wa baadhi ya miundombinu ya soko hilo.

Mstahiki Meya aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa Manispaa ya Kinondoni itayafanyia kazi changamoto zilizopo katika masoko hayo kwa haraka. Sheria hiyo ndogo Manispaa ya Kinondoni ya Masoko na Magulio ya Mwaka 2019 imefanya mabadiliko ya viwango vya tozo kwenye masoko yaliyo ndani ya Manispaa ya Kinondoni.

**LIPA TOZO KWA MFUMO TAUSI**



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza anawatangazia wananchi wote waliopewa viwanja maeneo ya Mabwepande na Nyakasangwe, kuwa wanatakiwa kulipia viwanja vyao mara moja.

NAMANGA

MWENGE
MIKOCHENI
BUNJU

KIBO HOUSE - TEGETA

# MATANGAZO MUHIMU KWA WANANCHI MANISPAA YA KINONDONI DIVISION YA KILIMO, UVUVI NA MIFUGO



**BI. HANIFA SULEIMAN HAMZA**
**Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bi Hanifa Suleiman Hamza anawatangazia wananchi wote waliopewa viwanja maeneo ya Mabwepande na Nyakasangwe, kuwa wanatakiwa kulipia viwanja vyao mara moja.

Kumbuka kuwa tarehe ya mwisho ya kulipia pamoja na nyongeza ya siku za kulipia mlizopewa zilikwisha. hivyo, iwapo utashindwa kulipia kiwanja chako ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya tangazo hili, utanyang'anywa kiwanja hicho na kitapangiwa mtu mwingine.

ili kufanya malipo hayo fika katika ofisi zetu zilizopo magomeni au katika vituo vyetu vya malipo vilivyopo:

- **KIBO HOUSE - TEGETA**
- **MWENGE**
- **MIKOCHENI**
- **NAMANGA**
- **BUNJU**

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA MANISPAA YA KINONDONI




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni anawatangazia wananchi wote waliopewa viwanja maeneo ya Boko Dovya (kwa somji) kuwa, mnatakiwa kulipia viwanja vyao mara moja.

Kwa wananchi wa salasala waliotambuliwa na kuhakikiwa wanatakiwa kulipa malipo yao haraka ili taratibu nyingine za upimaji na umilikishaji ziendelee.

Kumbuka kuwa hautakiwi kufanya maendelezo yoyote kabla ya kulipia au kumalizia kulipia kiwanja chako jambo ambalo ni kinyume cha sheria. kushindwa kulipia au kumalizia kulipia kiwanja chako kutapelekea manispaa kuchukua hatua dhidi yako.

Ili kufanya malipo hayo fika katika ofisi zetu zilizopo magomeni au katika vituo vyetu vya malipo vilivyopo:

- **Kibo house**
- **Tegeta; mwenge**
- **Mikocheni Namanga**
- **Bunju**

Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni

# MATUKIO KATIKA PICHA MANISPAA YA KINONDONI




***Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule(kushoto), Mkurugenzi Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza pamoja na Katibu Tawala Manispaa ya Kinondoni Bi. Stella Msofe wakikabidhi cheki ya bilioni 2.5 kwa vikundi 115 vya wafanyabiashara ndani ya Manispaa ya Kinondoni.***



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza ahimiza lishe bora kwa watoto mahuleni ili kuongeza ufaulu wao*



*Mkuu wa Wilaya Mhe. Saad Mtambule akiwa katika picha ya pamoja na maofisa wa Jeshi la polisiTanzania baada ya kukutana na kujadili masuala ya ulinzi na usalama ndani ya Manispaa ya Kinondoni.*



***Timu ya KMC wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali kutoka Manispaa ya Kinondoni wakiongozwa na Mkurugenzi Bi. Hanifa Suleiman Hamza pamoja na Naibu Meya Mhe. Joseph Rwegasira katika basi lao jipya.***




*Mstahiki Meya kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Mhe. Songoro Mnyonge.*



*Mstahiki Meya, Katibu Tawala, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Diwani wa Kata ya Mbezi Juu (Anna Lukindo} wakiwa katika picha ya pamoja.*



*Moja ya kundi la wazazi pamoja na viongozi wa dini wakipewa na kutoa ush-auri juu ya malezi bora kwa jamii inayowazunguuka wanakinondoni*



*Elimu ndio jadi yetu karibu Manispaa ya Kinondoni uapte elimu bora isiyo na malipo kutoka kwa watumishi maridsadi wa Usatawi wa Jamii*

Na ZIANA BAKARI

# MFUMO WA TAUSI KATIKA KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI



Moja ya mafanikio yanayopatikana katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ni kuendeleza mfumo wa kuwasaidia wafanyakazi katika kuendesha maisha yao vizuri.

Katika kuendeleza mafanikio yanayoendelea kupatikana katika Manispaa hiyo kuonekana kuzidi kukua kila siku kadri ya siku zinavyozidi kwenda.

Ofisa biashara ambaye ni mwekezaji katika Manispaa hiyo, Shadrack Francis, anasema hapo awali walikuwa na mfumo wa mapato wa kwanza ambao ulidumu miaka 7, ulikuwa unamuangalia mtoa huduma lakini katika mfumo wa tausi utaangalia mtoa huduma na mtumiaji wa huduma hiyo.

Pia, anasema kulingana na mfumo huo wa awali wa hapo mwanzo ulikuwa haugusi zaidi wananchi na kuufikia kwa wao kuutumia moja kwa moja namna ambavyo wataweza kuufikia mfumo huo kwa unahisi.

Hivyo basi anadokeza kuwa Mfumo wa mpya wa mapato wa Tausi ulioanzishwa mwezi Novemba mwaka jana na rasmi ulianza kutumika kwa wananchi mwezi Desemba mwaka jana, mfumo huu upo tofauti na ule wa awali, kwani utamsaidia mfanyabiashara popote alipo anaweza kuufikia na akapata huduma nzuri iliyobora na salama ili kutengeneza mahitaji yake.

Kwanini umeitwa Mfumo wa Tausi

Ofisa huyo anasema kuwa lengo kubwa la kuuita mfumo jina la Tausi linatokana na tausi mwenyewe ndege ambaye anasikia kuwa na sifa nzuri, mtanashati, mzuri wa kuvutia kwa rangi alizokuwa nazo na zote zipo katika bendera ya taifa.

Anasema kupitia rangi hizo inaonyesha ni alama na nembo ya taifa kiujumla, lakini Tausi ni mojawapo ya alama za utajiri, rasilimali na pia ni tunu.

Mbali na hayo, anasema kuwa Tausi huyo ambaye ana manyoya zaidi ya 200 ambayo yanasanifu na huduma ambazo watakazokuwa wanazitoa kwani ni nyingi na zaidi ya hizo.

Shadrack anasema, kulingana na namba ya manyoya yake yanasanifu vema huduma ambazo itapatikana kupitia mfumo huu unapaswa kuondoa taarifa ambazo zina hatari namna moja au nyingine zinaweza kuhatarisha mfumo kwa mtumiaji.

"Mfumo huu unajihami wenyewe kutumia mifumo itakayowekwa, lakini siyo hivyo tu mfumo huu unaweza kumuondosha yule anayetumia 'hack' au kuchukua taarifa za aina yoyote ile ambayo siyo ya kwake.

*Inaendelea Uk....18*

*Kutoka Uk 17......*

Ofisa huyo anaendelea kudokeza kuwa, ndege Tausi anaishi zaidi ya miaka 20 na hata katika mfumo huo una maisha marefu ambao wanaamini wataishi nao zaidi ya miaka 20 na kuendelea.

Pia, anasema kulingana na sifa za ndege huyo huwa ana tahadhariya mara zote za kuangusha majani yake na kujihami na hivyondivyo ulivyo mfumo huu.

Ofisa huyo anasema kuwa, mfumo huo ambao umeleta mafanikio makubwa katika utekelezaji wao na hata kwa huduma wanazozitoa hadi hivi sasa wanaendelea kuutumia kwa mafanikio makubwa ambayo yamewasaidia kuendeleza shughuli zao.

Anasema mfumo huo ambao umebeba huduma zote ambazo zinatolewa kwa ukusanyaji wa mapato katika huduma ya leseni ya biashara, kulipia vibanda masokoni, ada mbalimbali za masomo na hata huduma zingine mbalimbali.

Anasema kuwa jitihada zote zinatokana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo imeboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuendana na mabadiliko ya sheria na sera, kanuni na taratibu zinazohusu ukusanyaji wa mapato katika mamlaka ya serikali za mitaa.

Aidha, mfumo huo umezingatia mahitaji ya wadau mbalimbali pamoja na mabadiliko ya teknolojia, ambayo maboresho hayo yalilenga kuongeza ufanisi kama ifuatavyo

Faida za Mfumo huo

Anasema mteja anaweza kufanya malipo kwa kutumia VISA, Mastercard na Control namba kutoka GePC, hii kumsaidia mteja kutofika katika Halmashauri kuomba au kulipia tuzo, ushuru, leseni, faini au vibali hivyo anafanya mwenyewe kupitia dirisha la mteja.

Pia, mteja kumsaidia mteja kupata vibali vya ujenzi na leseni za biashara kwa njia ya mtandao na wakusanyaji wa mapato ya nje wa Halmashauri itawasaidia kupunguza matumizi ya fedha na huchelewa kupeleka fedha, benki na kutopeleka lauda fedha benti kwa wakusanyaji.

Anasema jukumu hili lipo kwa wakala na inasaidia kupunguza defaulters hata kwa wale wanaotumia matumizi ya nida katika msajiri wa mlipa kodi na watumiaji wa mfumo huo.

Anasema hii kusaidia kuwa na utambulisho mmoja wa mlipa kodi katika mfumo hata pale unapoomba huduma nyingine katika Halmashauri na huongeza usahihi na uadilifu wa watumiaji na matumizi ya TIN hii humsaidia katika biashara au kampuni.

Shadrack anasema kusaidia kuzitambua na kuzipa Ankara ya malipo ya biashara zote zinazotakiwa kulipa ushuru wa huduma kufuatia na utoaji wa leseni ya biashara na husaidia kusimamia mkataba kwa njia ya kieletroniki.

Anasema mikataba ya mawakala wa ukusanyaji wa mapato, kwa kutumia (collectors) vizimba vya Halmashauri (House Rent) na husaidia kuuza na kununua viwanja vilivyopimwa na Halmashauri njia ya kieletroniki.

husaidia kutambua matumizi ya GIS katika kutambua maeneo ya ukusanyaji (Pos collection Areas) na walipakodi kujua kaya zilizokaribu taka ngumu na nyumba wanapoishi, kwa msaada unaweza kupiga simu namba +255 735 160 210 barua pepe huduma@ tamisemi.go.tz

Walengwa wa mfumo

Ofisa huyo anasema walengwa katika mfumo huo ni wananchi hasa wafanyabiashara nchini kwa kuangalia matumizi ya leseni za biashara kuanzia katika maombi.

"Mfumo huu una njia kuu mbili za kujisajili hivyo mtumiaji anapaswa kuchagua njia mojawapo, njia ya kutumia mfumo wa maswali na njia ya kutumia nywila mahususi One Time Password (OTP).

Aidha, anasema muitikio ni mkubwa tangu walipoanzisha mfumo huo wa Tausi mwaka jana, kuanzia mwezi Januari hadi hivi sasa wameweza kusajili leseni za biashara 350 kwa Manispaa ya Kinondoni.

Shadrack anasema ni vema elimu kuendelea kutolewa kwa wananchi kuweza kuwasaidia kujua mfumo unaendeshwaje Kuanzia kujiunga hadi kuanza kuutumia.

"Manispaa ya Kinondoni imeanzisha vituo sita vya mapato ambavyo vipo Magomeni, Mwenge, Mikocheni, Msasani, Bunju na Tegeta Nyuki, kupitia vituo hivi tunaamini wakazi wa Manispaa ya Kinondoni wataweza kupewa elimu ya kujiunga na mfumo huo.

"Wito wangu kwa wananchi huu mfumo ni rahisi kwao kuutumia, mfumo huo utampa maelezo kwa lugha ya kiswahili na Kingereza hivyo nitoe rai kwa wananchi kama kutakuwa na tatizo lolote fika mara moja katika vituo yetu kuweza kupata huduma ilikuwa bora na elimu ya kutosha,"anasema Shedrack.

***Lipa Kodi kwa Manufaa ya Manispaa yako***

# KINO BOY'S

*Karibuni viwanjani leo*





# USHINDI NDIO JADI YETU WANAKINO BOY'S



Tunaendelea kuboresha timu yetu ili tuendelee kuwa juu muda wote

Kwasasa tumeanza na ununuzi wa basi jipya ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza changamoto mbalimbali kwa wachezaji wetu.

KMC FC (KINO BOY'S) ni yetu sote HATUFIKILII KUSHUKA DARAJA

## TAKWIMU ZA KMC 2022/2023

**MECHI - 23**

**POINTI - 23**

**NAFASI - 12**

**MICHEZO ILIYOBAKI - 7**

KMC FC imefanikiwa kuvuna mashabiki zaidi ya 1,000 kutoka ndani ya Kata 20 pamoja na nje ya masniapaa ya Kinondoni

**KMC NI YETU SOTE**




LA KIMATAIFA

# HAKUNA TIMU KUBWA ZAIDI YA KMC FC

**Na KMC MEDIA**




Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Bi Hanifa Suleiman Hamza, amewatoa hofu wachezaji wa KMC FC kuwa hakuna Timu ya Soka kubwa zaidi yao.

Bi. Hanifa ameyasema hayo alipokutana na baadhi ya viongozi wa Timu hiyo walioambatana na Kikosi cha KMC FC Leo katika Ukumbi wa Manispaa.

"Hakuna Timu kubwa zaidi yetu, tunaweka Mazingira mazuri na Bora zaidi kwa Timu yetu kuweza kufanya vizuri," alisema.

Aliwaeleza wachezaji hao kuwa KMC FC kwa Sasa imepata Bus kubwa ambalo litawawezesha wachezaji kusafiri vizuri. aliongeza kuwa, " tutakuwa Timu ya Pili kuwa na Uwanja Mkubwa wenye vifaa vya kisasa." Manispaa ipo kwenye hatua za ukamilishaji Uwanja wa Mpira uliopo Mwenge, Jijini Dar es Salaam.

Naye Naibu Meya wa Manispaa hiyo, Mheshimiwa Josephat Rwegasira, aliitaka Timu hiyo kuhakikisha inafanya vizuri katika mechi zake Nane zilizobaki.

Mheshimiwa Rwegasira alisema, "KMC FC Ni sura ya Manispaa ya Kinondoni, tupo tayari kutoa Fedha kwa ajili ya Maendeleo yake."

Kwa upande wao Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Timu hiyo walimpongeza Mkurugenzi kwa mwelekeo wake wa kuboresha Mazingira ya timu.

Nao baadhi ya wachezaji wamemshukuru Bi. Hanifa kwa kuwawezesha kupata Bus kubwa litakalo wawezesha kusafiri mikoani bila kuchoka.



# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI








**Jarida la Manispaa ya Kinondoni 2 2023**

***www.kinondonimc.go.tz***